BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 04 Juni, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2025/2026.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

38. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

    Uharibifu wa mazingiria duniani umeupelekea Umoja wa Mataifa kupitia taasisi zake kuanzisha mifuko mbali mbali kama vile 'Climate Investment Funds (CIF), Global Environment Facility (GEF) na Green Climate Fund (GCF)' ili kukabiliana na athari kwa nchi zinazoendelea na visiwa kama Zanzibar.

(a) Ni kwa kiasi gani Zanzibar imefaidika na fedha zinazotoka katika mifuko hiyo.

(b) Kwa kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT), ni kiasi gani cha fedha ambacho Zanzibar inakipata kutoka katika mifuko hiyo.

(c) Ni miradi gani mikubwa ya kimazingira imefanyika Zanzibar kupitia fedha za mifuko hiyo.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

75. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna maeneo mengi ambayo wanaishi askari wetu na kulala katika majengo waliyotengewa kwenye kambi ambazo wanalinda usalama wa nchi na raia wake.

Kuna utaratibu upi wa kuwapatia majengo bora askari wetu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

34. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji nchini ambapo visiwa vingi vimepata wawekezaji na wameanza kuwekeza, bado jamii haijafaidika na miradi ya Corporate Social Responsibility (CSR) kutoka kwa wawekezaji hawa.

(a) Ni miradi mingapi ya uwekezaji imefanyika nchini tokea 2020.

(b) Ni ipi sera ya Serikali juu ya CSR kwa wawekezaji wanaowekeza Zanzibar.

(c) Ni miradi mingapi ya CSR imewafikia wananchi wa Zanzibar.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

203. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Ni aina gani ya vipindi kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) ambavyo vina muktadha mzima wa kutoa elimu na uelewa wa maarifa kwa jamii.

(b) Ni vipindi gani na vipi vinalenga kutoa burudani.

(c) Ni aina gani ya vipindi vinaibua matatizo ndani ya jamii.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

264. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi yamesaidia vipi kukabiliana na uzaaji na uvamizi wa wadudu waharibifu wa mazao na kuongeza uzalishaji nchini.

289. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Dhana ya kilimo cha umwagiliaji inaweza kushushwa chini kwa wakulima wadogo wadogo wanaofanya shughuli za umwagiliaji pasipo kuratibiwa na Wizara (Idara ya Umwagiliaji), na hivyo kuhudumiwa na makampuni binafsi ambayo hutoza gharama kubwa kwa wakulima.

Ni lini Wizara yako itakianzisha Kitengo cha Umwagiliaji Binafsi (Private Irrigation Department) ili kuratibu na kuwahudumia wakulima wenye kuendesha shughuli za umwagiliaji katika maeneo yao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

137. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na malalamiko ya kituo cha Mnyanjani Tanga kuwa hakipo kwenye mazingira mazuri ya kiusalama, pamoja na kupotea baadhi ya alama zilizowekwa za kuonesha maeneo yaliyopita umeme kuelekea baharini.

(a) Je, suala hili lina ukweli wowote.

(b) Kama lina ukweli, Je Wizara inalichukulia hatua gani ya kuondosha tatizo hilo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

259. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kupanga, kupima na kumilikisha ardhi sio tu inaondosha au kuipunguza changamoto ya migogoro ya ardhi bali pia inasaidia kwa kiasi kikubwa kupandisha hadhi ya ardhi tuliyonayo.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imefanikiwa katika upimaji na umilikishaji wa ardhi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

232. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Inasemekana mradi wa ujenzi wa barabara za ndani kwa Unguja na Pemba hautahusisha ujenzi wa madaraja makubwa kwa mujibu wa mkataba husika.

(a) Je, kuna ukweli upi wa suala hili.

(b) Je, hatma itakuwaje kwa zile barabara zenye kiwango kikubwa cha maji iwapo hazitajengewa madaraja makubwa.

310. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane chini ya uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi imefanya kazi nzuri ya kujenga barabara za kisasa Zanzibar. Barabara hizo zinaleta haiba nzuri ya nchi yetu hata hivyo barabara hizo zinawekwa alama za zamani za barabarani.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka alama za kisasa za barabarani zenye mfumo wa kidijitali na kuondokana na alama za zamani.

(b) Kwa kuwa nchi nyengine zimekuwa na taa za kuongozea gari (traffic lights) za kisasa zinazoweka muda wa kuongozea gari, je, ni lini Serikali itaweka taa za aina hiyo ili kuzidi kuleta haiba nzuri ya barabara zetu.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

142. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Upungufu wa damu mwilini umeonekana kuwa ni tatizo kubwa kwa kinamama wengi waja wazito.

Wizara inachukua jitihada gani katika kukabiliana na tatizo hili.

<u>**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**</u>

251. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, Serikali inadhibiti vipi uchafuzi wa mazingira baharini kutokana na meli zinazomwaga mafuta baharini.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

49. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli za Serikali za 'boarding' zinafanya kazi kubwa ya kuwasaidia vijana wetu kupata ufaulu mzuri na kuongeza ubora wa elimu kwa Zanzibar. Pamoja na juhudi hizi skuli hizi zinakumbwa na uhaba mkubwa wa makaazi, vyakula na huduma nyengine.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inafahamu kwamba skuli hizi zinawatoza wazee fedha kwa ajili ya vyakula na huduma nyengine kila mwezi.

(b) Je, ni bajeti ya kiasi gani hupelekwa na Serikali kwa skuli hizi za 'boarding' ili kuendana na sera ya elimu bila ya malipo.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha skuli zote za 'boarding' zimepatiwa makaazi kwa ajili ya wanafunzi kabla ya kuifanya skuli husika kuwa na 'boarding'.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa nini na kwa vipi jengo la Jamatkhani linaingia katika orodha ya majengo yanayobeba vielelezo muhimu sana katika historia ya Zanzibar.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2025/2026.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**04 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**